38. Chunguza kwa makini mchoro ufuatao hapo chini unaonesha sehemu za uzazi wa kiume. Herufi G inawakilisha:-




(A) Urethra
(B) Mirija ya manii
(C) Korodani
(D) Ureta
(E) Korodani

39. Yafuatayo ni makundi ya mimea yanayojumuisha mimea jamii ya mikunde (A) Karoti, nyanya, vitunguu na njegere (B) Bamia, hoho, njegere na kunde (C) Mtama, uwele, maharage na mahindi (D) Mahindi, ulezi, mtama na uwele (E) Njugumawe, maharage, njegere na kunde

40. Badiliko la kikemikali hutokea pale panapokuwa na badiliko la___(A) Maji kuganda na kuwa barafu (B) Maji kuwa mvuke (C) Mvuke kuwa gesi (D) Kunapotokea badiliko jipya la maada (E) Mwanga unapoakisiwa

## SEHEMU B: JAZA NAFASI WAZI

41. Kizingiti cha mgando cha sentigredi ni O, je kizingiti cha mgando cha Farenhaiti ni nyuzi ngapi?_________________

42. Chunguza kwa makini mchoro ufuatao hapo chini kisha tafuta thamani ya G




43. Chunguza mchoro ufuatao hapo chini. Mchoro huo unawakilisha aina gani ya transfoma? ___________________




44. Elimu inayohusu viumbe hai na mazingira yao huitwa________

45. Mfupa mrefu kuliko yote katika kiunzi cha binadamu ni_______

# HALMASHAURI YA JIJI LA ARUSHA

**MTIHANI WA KUJISOMEA NYUMBANI KWA DARASA LA SABA 2020**

**SOMO: SAYANSI**

**MUDA: SAA 1:30 JUNI 2020,**

**MAELEKEZO**

1.Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali **arobaini na tano (45)**
2.Jibu maswali **yote** katika kila sehemu.
4. Andika **jina lako, shule na somo kwa usahihi katika karatasi yako ya kujibia.**

## SEHEMU A: CHAGUA JIBU SAHIHI ZAIDI

1. Sehemu ya jicho inayopokea miale kutoka kwenye lenzi na kuunda taswira (A) Mboni (B) Kornea (C) Retina (D) Pupil (E) Kope
2. Ni sehemu ya ua inayovutia wadudu (A) Mizizi (B) Petali (C) Pistili (D) Tunda (E) Mbegu
3. Tezi inayotoa ushauri wakati mtu anapokabiliwa na hatari katika mfumo wa homoni (A) Pituitari (B) Kongosho (C) Medula (D) Adrenali (E) Thairoidi
4. Upungufu wa damu mwilini hujulikana kama ___(A) Anemia (B) Pumu (C) Selimundu (D) Kisukari (E) Kiseyeye
5. Wingi wa umeme katika mkondo hupimwa na chombo kiitwacho____(A) Voltimita (B) Ampia (C) Electroni (D) Ohmu (E) Ameta
6. Ili moto uwake ni lazima pawepo na____(A) Haidrojeni (B) Kabonidioksaidi (C) Nitrojeni (D) Laktojeni (E) Oksijeni
7. Uwepo wa unyevunyevu na Oksijeni katika chuma husababisha___ (A) Chuma kuyeyuka (B) Chuma kupata kutu (C) Chuma kusinyaa (D) Badiliko la kiumbo (E) Chuma kuwa sumaku
8. Matokeo ya mwisho ya protini katika uyeyushaji wa chakula mwilini ni____(A) Homoni (B) Kimeng'enyo (C) Asidi za amino (D) Amilesi (E) Faliko
9. Maada pekee inayoweza kubadilika katika hali zote tatu ni____ (A) Hewa (B) Maji (C) Mshumaa (D) Chuma (E) Karatasi
10. Hii ni mojawapo ya mashine tata____(A) Toroli (B) Mkasi (C) Baiskeli (D) Nyundo (E) Ndoano
11. _____Ni mojawapo ya ugonjwa wa kurithi (A) Malaria (B) Hemophilia (C) Covid-19 (D) Kipindupindu (E) Surua
12. Mwanga unapopenya media moja kwenda media nyingine huonesha sifa ipi? (A) Kusharabiwa (B) Kuakisiwa (C) Kutawanyika (D) Kupinda (E) Kubadilika rangi

13. Ateri kubwa kuliko zote ni_____(A) Palmonari (B) Vena kava (C) Pituitari (D) Ini (E) Aorta
14. Wafuatao ni kundi la mamalia isipokuwa _____(A) Nyangumi (B) Kangaroo (C) Popo (D) Tilapia (E) Panya
15. Mojawapo ya kundi la magonjwa yasiyoambukiza____
(A) Malaria, kansa, shinikizo la damu (B) Anemia, selimundu, surua
(C) Utapiamlo, kansa, kifua kikuu (D) Kansa, utapiamlo, ualbino, TB
(E) Kipindupindu, Kansa, tetekuwanga
16. Chombo kinachotawanya miale ya mwanga katika rangi zote saba______(A) Kioo (B) Lenzi mbinuko (C) Luninga (D) Prizimu (E) Spektamu
17. Kitendo cha mmea kutumia kabonidioksaidi na kutoa oksijeni wakati wa mchana_____(A) Eksiresheni (B) Fotosinthesisi
(C) Respiresheni (D)Haidrotropizimu (E) Transpiresheni
18. Waya mwembamba unaolinda vifaa vinavyotumia umeme dhidi ya hitilafu ya umeme ni_____(A) Saketi (B) Ampia (C) Fyuzi
(D) Adapta (E) Ukinzani
19. Joto la kawaida la mwili wa binadamu ni_____(A) $98.4^0C$
(B) $94.8^0C$ (C) $37^0C$ (D) $100^0C$ (E) $104^0C$
20. Si hitaji muhimu katika uotaji wa mbegu (A) Unyevu (B) Hewa ya oksijeni (C) Joto la kadiri (D) Udongo (E) Mbegu iliyokomaa vema
21. Yafuatayo ni makundi ya sayari isipokuwa_____(A) Dunia, zebaki, sumbula (B) Mars,zohali,sumbula (C) Satani, dunia, zebaki
(D) Jua, mwezi, satelaiti (E) Dunia, neptuni, utaridi
22. Mariamu amekula samaki, njegere na yai ni kirutubisho gani ameongeza mwilini?
(A) Vitamini (B) Wanga (C) Mafuta (D) Protini (E) madini
23. Kompaundi inayopatikana kwenye damu inayosaidia damu kuganda pindi mtu anapopata jeraha ni_____(A) Chembechembe nyeupe za damu (B) Uteute wa damu (C) Chembe chembe nyekundu za damu
(D) Chembe sahani (E) Plasma
24. Fomula ya kemikali ya maji ni____________________
(A) $O_2$ (B) HO (C) $HO_2$ (D) $H_2O$ (E) 2HO
25. Nazi hutawanywa kwa njia ya_____(A) Wanyama (B) Upepo (C) Maji
(D) Binadamu (E) Wadudu
26. Alama ifuatayo kwenye sakiti ya umeme huwakilisha____



(A) Fyuzi (B) Waya (C) Soketi (D) Taa ya umeme (E) Kikinza
27. Sehemu ya mmea inayohusika na uzazi ni______(A) Majani (B) Mizizi
(C) Ua (D) Shina (E) Mbegu (F) Mishipa
28. Sehemu ya sikio inayowakilisha sikio la nje_____(A) Koklea
(B) Nyundo (C) Vifereji vya nusu duara (D) Pina (E) Kikoko
29. Shangazi ana tatizo la kuona mbali, anashauriwa kuvaa miwani yenye lenzi_____(A) Mbinuko (B) Bapa (C) prizimu (D) Mbonyeo (E) Nyingi
30. Kukosa pumzi, kubanwa na mbavu, kukohoa, mafua makali na homa ya mapafu hizi ni dalili za______(A) Malaria (B) Pepopunda
(C) Covid-19 (D) Kipindupindu (E) UKIMWI
31. Badiliko la kiumbo ni lipi kati ya haya yafuatayo______(A) Chuma kupata kutu (B) Tunda kuoza (C) Ndizi kuiva (D) Mshumaa kuyeyuka (E) Kuungua karatasi
32. Vifuatavyo ni vyanzo vya umeme isipokuwa:- (A) Maji (B) Seli kavu
(C) Mti (D) Jua (E) Jenerata
33. Ugonjwa wa COVID-19 husababishwa na_____(A) Bakteria
(B) Protozoa (C) Plasmodia (D) Kuvu (E) Virusi
34. Chunguza mchoro ufuatao kisha taja sehemu zilizooneshwa kwa herufi C, G na E




A. Petali, kichavua na ovuli (B) Kichavua, stigma na filamenti
(C) Petali, stigma na ovuli (D) ovuli, sepali na ovuli
(E) Petali, kichavua na stigma
35. Saketi kamilifu ni lazima iwe na kitumizi, swichi, waya na______
(A) Chanzo (B) Nguzo (C) Radi (D) Luku (E) Kikinza
36. Mlishano sahihi katika kundi hili ni upi_____
(A) Majani → Swala → Simba
(B) Majani → Simba → Swala
(C) Simba → Swala → Majani
(D) Swala → Majani → Simba
(E) Simba → Majani → Swala
37. Ufuatao ni mchoro rahisi wa mzunguko wa damu mwilini. Mishipa ipi miwili inayosafirisha damu yenye oksijeni




(A) E na F (B) G na H (C) F na H (D) E na G (E) E, F na G